

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

SHULE YA SEKONDARI IKAMA

S. L. P 630,

KYELA

05 /12 /2020

MWANAFUNZI

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IKAMAWILAYA YA KYELA

MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.

1.0 Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.shule hii ipo umbali wa meta 200 toka barabara kuu ya kyela-ipinda.Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021.Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo hiyo, Mwisho wa kuripoti ni siku saba tu.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

- a) Sare ya shule ni rangi ya **kahawia** na **kijani kikavu** kwa wavulana.
Kwa wasichana washone suruali rangi ya **kahawia** na sketi rangi ya **kijani kikavu**.
- b) Mashati mawili(2) meupe ya mikono mifupi kwa wavulana.
- c) Wasichana washone brauzi ya kisolo cheupe kimoja na shati moja la mikono mifupi.
- d) Viatu vyeusi vya ngozi jozi MBILI(2) vyenye kamba kwa wote.
- e) Soksi NYEUPE jozi tatu kwa wote.
- f) Sare ya michezo kwa shule hii itakayotumika siku ya juma tano itakuwa ni T-shirt ya zambarau iliyokolea (dark purple) inayoweza kupatikana shuleni kwa gharama ya Tshs. 10,000/=
- g) Daftari kumi(10) kubwa(kaunta QUARE3) kalamu,na mkebe wa hesabu.
- h) Kila mzazi wa mwanafunzi anatakiwa kuchangia chakula pindi mwanafunzi awapo shuleni kwa siku za masomo kama ifuatavyo;
 - i. Tsh. 2500/= kwa mwezi (elfu mbili na mia tano tu).
 - ii. Sado moja ya mahindi kwa mwezi.
 - iii. Kimbo tatu za mchele kwa mwezi.
 - iv. Kimbo tatu za maharage kwa mwezi.

ZINGATIA;

Wavulana hawatakiwi kushona suruali **modo** wala kuvaa **mlegezo**.

3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

3.1 shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978 .Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamna ya elimu nchini .Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maaandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu.
- c) Kuwahi na kutii kufanya kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- e) Kutunza usafi wa mwili wako na mazingira ya shule
- f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa .
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- h) Baada ya orientation course mwanafunzi hataruhusiwa kuongea /kuzungumza Kiswahili ama lugha yoyote isiyo rasmi.

3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZA SHULE

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo
4. Uvutaji bangi.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau bendera ya Taifa.
9. Kuo au kuolewa.
10. Kupata mimba, kutoa mimba au kumpa ujauzito mwanafunzi au msichana na mwanamke yeyote ndani na nje ya mipaka ya shule.
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi

NB: MEDICAL EXAMINATION FORM UTAPATIWA HAPA SHULENI MARA TU BAADA YA KURIPOTI.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII YA IKAMA

.....

F.M. PAUL

MKUU WA SHULE